MEDIA BRIEFS FOR MoM 10 JUNE, 2019

HABARILEO

- **Madini yaingiza Bil 4 kwa siku 75**

Masoko ya Madini nchini yameingiza zaidi ya Sh bilioni 4 katika kipindi cha siku 75 tangu yaanze kufunguliwa Machi mwaka huu. Kufunguliwa kwa masoko hayo kunatokana na agizo la Rais John Magufuli la kutaka kila mkoa ambako kuna shughuli za uchimbaji wa madini kufungua soko ili kuwarahisishia wachimbaji wadogo kuuza madini yao, lakini pia kudhibiti tatizo la utoroshaji wa madini uliokuwa ukifanywa hapo awali. Soko la kwanza kufunguliwa lilikuwa Soko Kuu la Dhahabu mkoani Geita ambalo lilifunguliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Machi 17 mwaka huu. Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Madini, Profesa Simon Msanjila alisema mpaka ilipofika Mei 30, mwaka huu, jumla ya masoko 26 ya madini yalikuwa yamefunguliwa katika maeneo mbalimbali...Kuhusu ufanisi wa masoko hayo, alisema hadi Mei 31, mwaka huu, jumla ya Sh bilioni 3.85 zilikuwa zimekusanywa kutokana na mrabaha,Sh milioni 64.25 kutokana na asa ya ukaguzi na shmilioni 76.86 kutokana na ushuru wa huduma. (Uk.1&3).

- **Umeme wakwamisha uzalishaji mgodi wa dhdhabu Chunya**

Ukosefu wa umeme wa uhakika umetajwa kuwa changamoto kubwa inayokwamisha uzalishaji kwenye mgodi wa dhahabu kwenye leseni namba PML 0000829SWZ uliopo wilayani Chunya mkoani Mbeya. Hayo yalibainishwa na Meneja wa Mgodi huo, Shingo Kimogele kwenye ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Albert Chalamila aliyezuru akilenga kujua uzalishaji unaofanyika mgodini hapo.Kimogele alisema kwa muda mrefu sasa wamekuwa na changamoto ya umeme wa uhakika, hali iliyosababisha shughuli za uzalishaji na nyinginezo kutokuwa za uhakika.(Uk.4)

NIPASHE

- **Habari katika picha-** Meneja wa Kampuni ya KNAUF Tanzania Ltd,Gergios Zachopoulos, akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa Kamishna wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula, wakiwa kwenye eneo la machimbo. (Uk.24).

MAJIRA

- **Wizara kuwaogezea uwezo wathaminishaji wa madini**

Naibu Waziri wa Madini Stanslaus Nyongo ameahidi kulifanyia kazi ombi la uhaba wa wataalamu wauthaminishaji wa madini ya almasi na vito nchini. Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea katika ofisi za Benki Kuu ya Tanzania ili kujionea shughuli ya uthaminishaji wa madini ya almasi yenye uzito wa karati **56,858.75** yaliyozalshwa kutoka Mgodi wa Williamson Diamond uliopo Shinyanga. Nyongo alisema wizara itatafuta namna ya kuhakikisha inawezesha kada hiyo kupata wataalam wa kutosha ikiwa ni pamoja na kutafuta wafadhili watakaoweza kugharamia mafunzo ya wataalam hao. (Uk.2).

- **Habari katika picha-** Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula, Kamishna wa Tume ya Madini Prof. Abdulkarim Mruma, mwenyekiti wa wachimbaji wadogo mkoa wa Lindi, Peter Ludovick na Mhandisi kutoka Tume ya Madini Fadhili Kitivai wakitoka kukagua machimbo ya madini ya gypsum ya kampuni ya KNAUF Tanzania Ltd mkoani Lindi mwishoni mwa wiki. (Uk.2)

- **Wachimbaji wa madini Lindi watoa kilio Tume ya Madini**

Mwenyekiti wa Tume ya Madini Prof. Idris Kikula amekutana na kilio cha wachimbaji wa madini mkoani Lindi kuhusu ongezeko la tozo kinyume cha sheria ya madini. Wakizungumza kwa nyakati tofauti mwishoni wa wiki, wachimbaji hao walisema halmashauri za wilaya na vijiji zimekuwa zinawatoza tozo zaidi na ile iliyowekwa na sheria mama ambayo ni 0.03 badala yake wamekuwa wakitumia ndogo (by law) zilizopitishwa na baraza ka

madiwani kuwatoza tozo zaidi kinyume na sheria mama.(Uk.2)

MWANANCHI

- **Mgodi waua watano, naibu waziri aagize ufungwe**

Naibu Waziri wa Madini Stanslaus Nyongo ameagiza kufungwa kwa mgodi wa dhahabu katika kijiji cha Kilama Iyengwe kilichopo Gairo, Morogoro ambao umesababisha vifo vya watu watano. Watu hao walifariki baada ya kufukiwa na kifusi katika machimbo hayo yanayodaiwa kufunguliwa kinyume cha sheria na utaratibu katika tukio khilo, wengine watano walijeruhiwa. Akizungumza na wachimbaji wadogo waliokutwa modini hapo jana, Naibu Waziri Nyongo alisema wanapaswa kufahamu kuwa ardhi yote ni mali ya serikali. (Uk.4).

- **Habari katika picha-** Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dk. Steven Kebwe, akisaidina na wachimbaji wadogo kuwatafuta wenzao waliofukiwa katika machimbo ya madini ya kijiji cha Kilama, Iyongwe, Gairo. (Uk.4)

DAILYNEWS

- **News in Photo-** Mining Commission Chairman Prof. Idris Kikula pictured in Mtwara yesterday inspecting a machine used in the screening of minerals. Right is a member of the commission, Prof. Abdulkarim Mruma. (Uk.2).

MEDIA BRIEFS FOR MoM 09 JUNE, 2019

TANZANITE

- **DC Logido akaribisha wafanyabiashara wa madini**

Mkuu wa Wilaya ya Longido Frenk Mwaisumbe amewakaribisha wafanyabiashara wakubwa wa Madini (Deaelers) katika soko la Madini lililofunguliwa hivi karibuni katika Mpaka wa Namanga wilayani Longodo Mkoani Arusha. Akiongea ofisini kwake amedai kuwa soko hilo litawaeahisishia wafanyabiashara hao wakiwemo wachimbaji kuuza madini yao kwa thamani halisi iliyopo na kuepuka kupunjwa na mabroka wenye nia ya kujinufaisha. (Uk.7)

MZALENDO

- **Soko la madini lapaisha mapato serikali 2018/19**

Zikiwa nimebaki siku 22 kufungwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, imeonyesha kwamba mapato ya serikali yamevunja rekodi na kufikia makusanyo ya Sh bilioni 311.33 tofauti na lengo ambalo lilikuwa ni sh bilioni 310.32. Kupanda kwa mapato hayo kunatokana na kuanzishwa kwa masoko ya madini kukunali mwelekeo wa serikali wa kulipa kodi ya madini, kuondoa kodi a mbazo zilikuwa ni changamoto. Hata hivyo, serikali imesema hadi kumalizika kwa mwaka huu wa fedha, inatarajia kukusanya sh bilioni 340 katika mapato yake, tofauti na lengo walilokuwa wamejiwekea. Kauli hiyo ilitolewa jana na Katubu Muuu wa Wizara ya Madini Profesa Simon Msanjila, alipozungumza na MZALENDO baada ya Msemaji wa Serikali Dkt. Hassan Abbas, kuandika katika ukurasa wake wa twitter hukusu wizara hiyo kukusanya mapato makubwa kuliko wakati wowote tangu uhuru mwaka 1961. (Uk.1& 3).